MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Cheche za Fikra

JUZUU 10 TOLEO 39

MEI 13, 2009

KIJARIDA CHA BURE— UKISHASOMA MPE MWINGINE—USIBANIE!

UCHAGUZI MDOGO BUSANDA

ISHARA TOKA MAGHARIBI

CM IKO MATATANI?



(Zitto kwenye kampeni Busanda)

Na. M. M. Mwanakijiji

Kwa vile jimbo liliwahi kuwa chini ya chama fulani haina maana kuwa jimbo hilo unapotokea uchaguzi mwingine basi liachiliwe ili chama hicho kilishikilie tena. Kama mawazo ya namna hiyo yangekubalika basi wapinzani wasingegombea Mbeya Vijijini na CCM wasingeenda kugombea Tarime.

Katika uchaguzi mdogo unaokuja huko Busanda kuna watu ndani ya CCM wakiongozwa na Katibu Mkuu wa CCM Mzee Makamba wanaoamini kwa makosa kuwa CCM wana hati miliki ya jimbo la Busanda na hivyo ni lazima wacha **(Inaendelea Uk.2)**



Benjamin. G. Mwalukasa
Mhariri

Kijarida Ulichoshika

- **Kinatoka kila Jumanne**
- **Ni cha bure kabisa!**
- **Kisichofungamana na chama chochote au fisadi yeyote!**
- **Kiko huru, kinathubutu, na hakiogopi mtu au hoja yoyote.**
- **Ni kijarida chako!**
- **Haki zote za kuchapa na kunakili zimeruhusiwa!**

Ndani ya Toleo Hili

Ishara toka Magharibi	1,2
Mhariri: Rostam hatajwi?	1,2
Zitto ahutubia Busanda	3
Zitto ahutubia Busanda	4
Riwaya ya Mwanakijiji	5
DaJessy: Kujiandaa ndoa	5
Picha, Katuni na Maoni	6

TAHARIRI:KUTAJWA ROSTAM NONGWA?

Alizomewa Rais mstaafu na kuitwa fisadi; kukawa kimya. Walitajwa kina Chenge, Mramba na Yona, kukawa kimya; Alitajwa Katibu Mkuu Hazina Gray Mgonja na Katibu Mkuu Ulinzi Vincenti Mrisho, kukawa kimya;

Alitajwa Kikwete pale Mwembe Yanga tena na Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kukawa kimya!

Ametajwa Rostam! Imekuwa nongwa. Taifa zima tunatakiwa kutetemeka na kupatwa na wehu kwa sababu amenyoshewa kidole hadharani.

Yaani, mara tatu serikali karibu mara karibu sita ndani ya siku chache wakasimama mawaziri, DCI, DPP, Makamu wa Rais n.k wote wakichukua upande wa RA.
Kwanini? Mwisho wamekuja na tamko la kushangaza kabisa asili yake. Rostam hatajwi? Tuambiane mapema.

ISHARA TOKA MAGHARIBI

guliwe kwani Jimbo hilo lilikuwa "lao".

Dalili za mwelekeo wa uchaguzi huo mdogo unaofanyika siku chache zijazo zinaonesha kuwa upepo wa mabadiliko unavuma kwa kasi zaidi huko magharibi na yawezekana sehemu hizo ndizo zitaongoza katika kuiangusha CCM na kwa mara ya kwanza kuiadhibu kutokana na kutotimiza ahadi zake, kulea mazingira ya ufisadi nchini na zaidi sana kuwasahau watu wa magharibi kwa miongo mingi tangu Uhuru! Hii itakuwa ni ishara kutoka magharibi.

CCM haina hati miliki ya jimbo la Busanda na ahadi ambazo wanazitoa leo hii wangekuwa wamezitekeleza miaka 40 iliyopita. Iweje leo ndiyo watoe ahadi za ume me, na "kuleta maendeleo" kana kwamba Busanda ilikuwa ni kisiwa kilichosahauliwa katika nchi ya kufikirika?

Ukweli ni kuwa CCM iko matatani Busanda, wao wanajua hilo, wapinzani wanajua hilo na wananchi wa Busanda wanalijua hilo Wanatambua kuwa kwa muda huu uliobakia kabla ya uchaguzi mkuu mwakani kinachofanywa na CCM ni ahadi ambazo hazimiziki mwaka huu, ni ahadi tu za kumlingishia mtoto pipi ili afanye kile ambacho mzazi anataka kufanya.

Ishara hii kutoka magharibi itaonekana kwa sababu wananchi wa Busanda ambao wamezukwa na utajiri wa kila aina bado wanaishi na kutegemea "maendeleo" kutoka serikali kuu. Leo hii wanatambua kuwa chanzo cha matatizo yao siyo laana ya Mungu, wachawi, au mizimu bali ni uongozi mbovu na sera mbovu ambazo zimewarudisha nyuma. Kiukweli wanatambua kuwa kuichagua CCM tena ni kuizawadia kwa kitu ambacho haistahili.

Wakati wananchi na watumishi wengi wanahangaika na hali za maisha kuna kundi kubwa la watu ambao wamechota utajiri mkubwa wa nchi yetu na kuufanya kuwa wa kwao na uzao. Na tukiwauliza basi wanakasirika na kufura. Wananchi wa Busanda wamechoka na vitisho na maneno hayo.

Wanataka mabadiliko. Mabadiliko ya kwanza kabisa ni mabadiliko ya kifikra. Wanatambua kuwa Baba wa Taifa aliposema kuwa CCM siyo mama na kama ingeacha misingi yake angeweza kuiacha wanajua alikuwa anamaanisha nini.



Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto (Kushoto) Mhe. Lucy Nkya, akimnadi mgombea wa CCM Busanda, Bi. Lolesia Bukwimba.

Kwamba, mara zote nchi iko juu ya chama na iko juu ya mtu yeyote. Nchi ni ya kwanza kwani ndipo mahali pekee ambapo wana na mabinti zetu kwa haki wanaweza kukimbilia ulinzi wa utajiri wake na hifadhi ya maisha yao.

Hivyo, Busanda leo hii kama ilivyokuwa Tarime imetambua kuwa mabadiliko ni lazima. Ni mabadiliko ya kuleta fikra mpya za kiuongozi, fikra mpya za mwelekeo mpya. Wanajua ni nani wa kumchagua kwani wanajua chama cha mtu huyo na sera zake na uongozi wake hata kabla hajawa madarakani ni mfano.

Hivyo, kwa CCM kumsimamisha mtu ambaye hakubaliki kunawafanya wana CCM wampigie mtu kwa sababu ya chama na siyo kwa sababu watu wanamkubali. Hata hivyo, hata wana CCM wengine ambao wanatambua nguvu ya kura zao hawatamchagua mtu huyo kwani ni dhamira zao zitakazokuwa matatani.

Hivyo, uchaguzi huu wa Busanda hauhusu hisia, na vionjo, na kwa hakika hauhusu chama au vyama, unahusu maisha ya baadaye ya Jimbo la Busanda na wananchi wake. Ni nani ambaye kweli ataweza kuwapigia kelele Bungeni na ambaye atakuwa tayari pia kuweka maslahi ya taifa mbele kuliko ya chama chake. Ni nani atakuwa tayari kupigana na wapambanaji wengine katika vita hii dhidi ya ufisadi.

Hivyo, ni uchaguzi rahisi kwa wananchi wengi kwani katika hali duni ya maisha yao, na katika kusahauliwa kwao kuna kitu kimoja ambacho hawajakipoteza bado. Uhuru wao. Ndiyo uhuru huu ambao watautumia kumchagua kiongozi wanayemtaka hata kama CCM na vyombo vyake vya dola watasimama na kuwatisha kwa sauti kali na kuleta kundi la wapiga debe wake.

Ukweli ni kuwa Busanda imeamka na hailali tena. Endapo CCM watapoteza Busanda mwaka huu ndipo watajua ni kwa kiasi gani watahitajika tena kuwashawishi wananchi wa Busanda kuwakubali tena mwakani. Endapo watashinda, wananchi wa Busanda hawana mtu mwingine wa kumlaumu bali wao wenyewe na kile wanachokipata itakuwa ni kile wanachostahili.

Vinginevyo, nguvu yao iko katika siri ya kura ambayo hakuna mtu, diwani, mpambe au kiongozi yeyote wa CCM anayeweza kujua kura gani imepigwa na nani. Haiwezekani licha ya wasiwasi wa watu wengi. Kura ile ndiyo nguvu pekee ambayo watawala wanayo mikononi mwao na ni nguvu ambayo wananchi wa Busanda wataitumia vilivyo na hivyo kuliangazia taifa kile ambacho nakiita hapa kuwa itakuwa ni ISHARA KUTOKA MAGHARIBI!

Utakuwa ni mwanzo wa Chama cha Mapinduzi kuanza kukataliwa kuelekea 2010. Na Watanzania watawashukuru ndugu zao wa Busanda kwa kuonesha njia na kufungua pazia la mabadiliko.

KARIBU MWANAKIJIJI.COM

"HUU NI ZAIDI YA UCHAGUZI"

Hii ndio hotuba iliyotolewa na Naibu Katibu MKuu wa CHADEMA, Mh Zitto Kabwe . Tarehe ya Mei 09, 2009 baada ya maandamano makubwa yaliyotanguliwa na Bango lenye ujumbe " Karibu Zitto Kabwe, Karibu Obama wa Tanzania, Mwongoze Magessa Bungeni, huku mbele yake wakiwa vijana waliobeba jeneza lililozungushwa kitambaa cha kijani katika kata ya Katoro ambayo ndio kata yenye wapiga kura wengi takribani asilimia thelathini ya wapiga kura wote wa jimbo la Busanda.

Mtakumbuka matokeo ya uchaguzi wa mwaka 2005 kwa kura halali na zisizo halali yalikipa CCM ushindi wa wabunge 274 na CHADEMA wabunge 11.Lakini kwa kipindi cha miaka mitatu, wabunge 11 wa CHADEMA tumeweza kuhakikisha masuala mengi muhimu kuhusu mwenendo wa Taifa letu yanajulikana kwa Umma. Bila CHADEMA watanzania wasingejua ufisadi wa Buzwagi, EPA wala ufisadi wa Richmond uliosababisha serikali ya awamu ya nne kuanguka. Nasema kuanguka kwasababu kikatiba waziri mkuu ndio mwenye serikali. Kwahiyo serikali hii ni ya awamu ya nne na nusu.

Wananchi wa Busanda, Ingawa tupo wabunge 11, lakini CHADEMA tupo makini kukabiliana na utawala huu mbovu chini ya uongozi mahiri wa Naibu Kiongozi wa kambi ya upinzani bungeni,na Katibu Mkuu wa CHADEMA, Dr Willibrod Slaa. Hii ndio sababu kwanini tunaomba mtuongezee mpiganaji wa 12, ambaye si mwingine bali kijana wenu, msomi wetu, mwenye sababu za kutosha kwa mapambano haya, Finias Magessa.

Ndugu zangu wa Busanda, Uchaguzi huu sio uchaguzi wa Ilani za vyama. Uchaguzi wa Ilani za vyama ulikuwa mwaka 2005, ndipo vyama viliomba kura kwa Ilani , na CCM ikapata asilimia 86 ya wabunge pamoja na Urais. Mwenendo wa serikali ya CCM wote mmeouna. Wanasikitisha na kukatisha tama wananchi. Ndio maana ninawaambia, Ilani ya CCM ni ileile, kama kwa kuwapa wabunge zaidi ya 200 pamoja na Urais wameshindwa kuwatumikia, mnadhani mkichagua mbunge huyu mmoja wa CCM atabadilisha kitu? Ataongeza nini kama wenzake zaidi ya 200 wameshindwa ? Jamani CCM hawana nyongeza ya Ilani! Ni hivi hivi!

Ndio maana ninawaambia kwamba uchaguzi huu ni muhimu sana sio tu kwa nyie wakati wa Busanda, bali watanzania kwa ujumla. Ni kipimo. Ni kura ya maoni ambayo katika nchi nzima nyie watu wa Busanda ndio mmepata fursa hii ya kujibu. Mmepata fursa ya kuwaambia watawala tarehe 24, Mei mwaka huu kama mnakubaliana na mwenendo huu wa watala au hamkubaliani. Mnaridhika au hamridhiki.

Ukipigia kura mgombea wa CCM Mei 24, tafsiri yake ni kwamba unaridhika na mwenendo wa utawala wa CCM, na ukipigia kura CHADEMA maana yake ni kwamba ni unatuma 'signal' kwa watawala wetu kuwa hauridhiki na mambo yanavyokwenda katika nchi yako.

Rais Jakaya Kikwete alipokuwa kwenye kampeni aliahidi maisha bora kwa kila mtanzania. Na CCM ikaahidi kwenye ilani yake kwamba itapunguza idadi ya watu hawa masikini kabisa kwa asilimia 50%. Leo mwaka 2009, mwaka mmoja kabla ya mwaka wa uchaguzi 2010, Taarifa ya Hali ya umasikini inaonesha kuwa idadi ya watanzania wanaoishi chini ya kipato cha dola moja(shilingi 1300) kwa siku wameongezeka badala ya kupungua, na sasa wamefikia milioni12.7. Umasikini unapungua, au unaongezeka?

Hili ndilo Busanda mnalo Mei 24. Ukipigia kura CCM maana yake unakubaliana na mwenendo wa serikali ya CCM uliosababisha idadi ya masikini kuongezeka mwaka hadi mwaka.

Hii ndio maana ya uchaguzi huu. Ni uchaguzi wenu wakazi wa Busanda. Sisi tumekuja kuwawezesha tu. Tumekuja kuwaunga mkono mfanye maamuzi sahihi kwa niaba ya watanzania wengine ambao hawakupata fursa hii. Mkichagua CCM mtakuwa mmewaangusha watanzania. Watanzania wana imani kubwa na nyie mliochaguliwa na Mungu kupiga kura hii ya maoni!

Kwahiyo tarehe 24, Mei, Ukichagua CCM, maana yake ni kwamba unaunga mkono mwenendo wa serikali ya CCM kusababisha watanzania 4, katika kila watanzania 10 wawe waendelee kudumaa akili. Na ukimpigia kura Magessa wa CHADEMA, maana yake ni kwamba, unapinga , unakasirishwa na mwenendo huu. Jamani taarifa hizi hatuzitungi sisi! Wala hatuziandai sisi.

Haya ndio maswali CCM wakija muwaulize, ingawa sidhani kama watafanya mikutano ya hadhara mana nimesikia wanaogopa sana kuzomewa kwa uzembe na ufisadi wa serikali yao.

Nimesikia hapa mji mdogo wa Katoro, ambayo ni makao makuu ya jimbo hamna umeme. Hamna tofauti na Kasulu wala Kibondo mkoani Kigoma. Madhara ya kukosa umeme sio tu kwa wenye uwezo wa kuwa na umeme kukosa umeme, hali hii inasababisha gharama za maisha kuwa juu, kwasababu gharama za uzalishaji zinakuwa juu.

Kwahiyo ukienda kupiga kura tarehe 24, Mei, unapaswa kujiuliza kama unakubaliana au hukubaliana na mwenendo huu. Ukichagua CCM maana yake unaridhika kuona kwamba wakati miaka 48 iliyopita watanzania walikuwa na huduma ya umeme ilikuwa 15, ni sawa, na sio tatizo kwa leo Tanzania huduma ya umeme kuwa asilimia 12. Naukiipigia kura CHADEMA mana yake unatu ma ujumbe kwa watawala kwamba unaumizwa na hali hii. Haukubaliani na hali hii.

Njia pekee yaw ewe mkazi masikini kukataa hali hii ni kukataa kuipigia kura CCM. Ni kuipigia kura CHADEMA. Ni muhimu uone kama nafasi hii adimu kuwa muhimu sana kwako. Maana uchaguzi huu umefanyika kwasababu ya mipango ya Mungu. Na tunao amini katika Mungu, tunaamini kwamba mipango ya Mungu haina makosa. Na kila mpango una busara yake. Msituangushe kwakupewa fursa hii kabla ya miaka5 kukamilika.

Ninyi wilaya yenu ya Geita, mna utajiri wa dhahabu unaozalisha takribani wakia laki tatu na nusu kwa mwaka, ambazo ni sawa na bilioni 211 kwa bei ya sasa. Lakini utajiri huo hauna tafsiri yoyote kwa maisha yenu.

Baada ya vuguvugu la kupinga mikataba mibovu liliasisiwa na CHADEMA tangu sekeseke la Buzwagi, Leo Geita mnapata dola laki 2 kutoka mgodi wa dhahabu wa Geita (Geita Gold Mining-GGM). Kule Tarime, Halmashauri ile chini ya Uongozi wa

(Inaendelea Uk. 4)

Soma bure

HOTUBA YA ZITTO BUSANDA

CHADEMA, kwa kuamini kuwa wawekezaji wanatunyonya watanzania wakawaida kwasababu ya elimu duni, CHADEMA tuliamua fedha yote ile ipelekwe kusomesha watoto bure kwa shule za sekondari. Ni kweli fedha hizi ni kiduchu sana, lakini si haba. Sio sawa na kukosa kabisa. Sasa kama Tarime fedha hizi zinasomesha watoto. Nyie wilaya ya Geita fedha hizi zinakwenda wapi? Zinaishia kwenye warsha, vikao na makongamano ya madiwani.

Yote haya ni matokeo ya utawala dhaifu na usiowajali wa Chama cha Mapinduzi-CCM.

Tarehe 24 Mei, ukienda kupiga kura, ukichagua CCM, maana yake unakubaliana na utaratibu wa sasa wa CCM kutoa dola laki mbili kwa mwaka kwa halmashauri yako badala ya dola milioni mbili kama Kamati ya Bomani inavyotaka unufaike na madini. Kura yako ni alama! Ukienda ukampigia kura Magessa, maana yake unataka Serikali ya CCM itoe dola milioni mbili badala ya dola laki mbili kwa Halmashauri yako.

Ndio maana nawaambia kuwa uchaguzi huu wa Busanda ni wa kihistoria. Mnayo nafasi ya kuamua kuiangusha CCM, mnayo nafasi ya kutukataa. Sisi tupo wabunge 11. Lakini kazi tuliyoifanya kwa miaka hii mitatu tunaamini, kama mnaipenda nchi yenu mtatuongezea wabunge.

Tumpate mpiganaji wa 12, Ndugu yangu Finias Magesa. Mkituchagua mtakuwa mmetupa moyo, na itatusaidia kuongeza mapamabno zaidi. Lakini mkituangusha mtakuwa mnatuvunja moyo. Ni sawa na kutuambia kuwa mapambano yetu dhidi ya ulinzi wa rasilimali za madini na vita dhidi ya ufisadi ni kelele tupu.

Tumekuwa tukiwaambia watanzania. Mwenyezi Mungu hakudhmilia nchi hii iwe na watu masikini kiasi hiki. Hebu angalieni, Kanda ya ziwa imejaa dhahabu, Almasi, na Nickel. Kanda ya Magharibi imejaa Shaba, Mafuta na madini ya fedha. Kanda ya kati ya ina madini ya uranium yanayotumika kutengenezea mabomu ya nuclear, Kanda ya Pwani imejaa gesi na mafuta. Kanda ya kusini imejaa makaa yam awe. Kila kanda Mungu ameipa utajiri. Lakini masikini wamejaa juu ya ardhi tajiri. Kwanini msichukue hatua? Mimi ninawaambia. Njia pekee ya kutoka hapa tulipo kwanza ni kuikataa CCM.Ndio maana ninarudia! Uchaguzi huu ni zaidi ya uchaguzi. Ni kipimo kama mnaridhika au hamridhiki na mwenendo wa utawala wa namna hii.

Tarehe 24, Mei ukienda kupiga kura , ukichagua CCM maana yake unakubaliana na gharama za maisha kupanda. Ukichagua CHADEMA na Magessa maana yake unatuma ujumbe kwa watala kwamba



hakubaliani na kupanda kwa gharama za maisha.

Polisi mnapaswa kukumbuka kuwa ninyi ni watoto wa masikini kama sisi. Mkimtesa kijana wa Busanda, basi ujue kwamba na wewe kwenu mdogo wako anateswa na polisi mwenzako. Ukimtesa mama wa Busanda hapa, ujue kwamba polisi mwenzako anamtesa mama yako huko kwenu. Ukimtesa mzee wa Busanda, ujue na wewe wazee wako wanateswa na polisi wenzako huko kwenu.

Polisi wanapaswa kujua leo ni polisi, kesho raia. Hatutaki polisi waonee raia, ingawa hatutaki raia wavunje sheria.

Jamani polisi wa Tanzania ndio polisi wanaolipwa kidogo kuliko polisi wote katika nchi kumi na mbili za SADC. Nchi zingine kama Malawi ambazo uchumi wake unategemea tumbaku lakini polisi wake wanalipwa vizuri kuliko polisi wetu, Nchi yenye madini, ziwa, bahari, ardhi yenye rutuba, watu wenye moyo wa kufanya kazi na kila aina ya utajiri.
Tarehe 24, Mei mchague Magessa akutetee wewe mkazi wa Katoro, awatetee wakazi wa jimbo la Busanda. Awatetee wakazi wa mkoa wa Mwanza. Awatetee watanzania. Mkoa wa Mwanza una majimbo 11, yote mkaipa CCM. Kuna Kikao cha Kamati ya mashauriano ya mkoa, RCC, Nani atawatetea kwenye RCC ilhali mmejaza wabunge wa CCM humo?

Mimi nawaambia kutoka uvungu wa moyo wangu kwamba, wabunge wa CHADEMA hata tufanye kazi namna gain Dodoma, kama hamna 'mbwa' mkali Geita, Mwanza, mtaendelea kuibiwa tu!. Tunahitaji mbwa mkali ambaye akiona ufisadi kwenye Halmashauri, RCC na Serikali kuu aje kuwaambia. Tunahitaji mtu mwenye rekodi na tusiye na mashaka kuhusu dhamira yake ya kututumikia. Na katika wagombea hawa, hakuna Mwingine isipokuwa Magessa.

Hakuna mtu yeyote wa CCM ambaye akiwa mbunge anaweza kupinga ufisadi wa CCM ilhali wabunge wote wa CCM ni zao la ufisadi.. Labda apinge kwa unafiki wa makundi ndani ya CCM lakini sio kwa dhamira ya mapenzi ya mtanzania kwa nchi yake. Magessa amesoma sekondari Tosa Maganga, Zitto amesoma sekondari Tosamanganga.

Magessa amesoma shahada ya kwanza na kufanya harakati Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Zitto amesoma shahada ya kwanza na kufanya harakati Chuokikuu cha Dar es Salaam. Magessa amesoma shahada ya pili Ujerumani, Zitto Amesoma Shahada ya pili Ujerumani. Ninawaomba wananchi wa Busanda, mpeni nafasi kijana wenu Finias Maggessa.

Ninaamini Magessa ni Zitto na Zitto ni Magessa.

Mchagueni Magessa!

Soma Bure
hoja zenye nguvu

RIWAYA ZA MWANAKIJIJI ZUWENA: BINTI WA KITANGA – 3

(kutoka toleo lililopita)

Hakukuwa na mtu yeyeto mwingine aliyebakia hapo ufukweni.

Alinipa raha tena na safari hii ilikuwa ni zamu yangu kujibu mapigo yake. Tukaendelea kufanya mapenzi hadi yeye alipofika kilele, ndipo na mimi nikajiachia. Tukabaki tumekumbatiana hivyo huku tukifurahia upepo wa bahari ya Hindi.

Kwa mbali tuliona mtu mwenye tochi akija upande wetu. Tuliamka hapo na kuvaa nguo zetu na kuelekea hotelini. Tulikula chakula cha jioni pamoja. Kwenye saa tatu za usiku Zuwena aliondoka kurudi kwao.

* * *

Mapenzi yetu yaliendelea hivyo kwa muda wa miezi hiyo yote na siku za karibuni baada ya kugundua kuwa Zuwena ni mja mzito nilikuwa na hamu sana ya kukutana na familia yake. Wazazi wake nao walitaka wajue ni nani baba ya mtoto. Hakuwaambia ukweli mara moja alikuwa akiwazungusha zungusha. Tulikuabaliana aje kunichukua kunipeleka kwao maeneo ya New Nguvumali nikutane na wazazi wake. Niliona lolote litakalokuwa ni lazima tuweke penzi letu hadharani. Alikuwa anakaribia kujifungua na itakuwa ni jambo la maana kama atawaambia ukweli wazazi wake.

Siku moja kabla yake Zuwena alinipigia simu majira ya saa tatu za usiku huku akilia kwa nguvu. Aliniambia kuwa wazazi wake hawataki kukutana nami na wamemtaka avunje uhusiano wetu. Aliamua kuniambia ukweli kuwa yeye ni mtoto wa Shehe mmoja maarufu na tajiri sana wa Mkoa wa Tanga na hawakuwa tayari mtoto wao azae na Mkristu au kuolewa na Mkristu. Alikiri kuwa ananipenda na yuko tayari kuja kuishi nami na hayuko tayari kuacha wazazi wake kumchagulia mtu wa kumpenda. Nilijikuta na mimi naanza kulia. Nikamwambie asubiri kesho yake ili akipata nafasi niende kukutana pale Mariner's Inn karibu na Kituo cha Polisi cha Central Chumbageni. Ukweli ni kuwa hakusubiri kwani usiku wa saa sita, alitoroka nyumbani kwao akipewa usafiri na rafiki zake wawili ili wamlete kwangu.

Kwa bahati mbaya walipata ajali ya gari kwenye Mzunguko wa barabara ya Ishirini kwenye njia panda ya kwenye Makorola na ile inaelekea kiwanda cha Chuma. Marafiki zake wale wawili walikufa papo hapo. Zuwena alijeruhiwa vibaya na hali yake haikujulikana itakuwaje.

* * *

Mawazo yangu yalikatishwa na Daktari aliyeingia hapo akiwa na kibao cha kuandikia.

"Bwana Mwanakijiji?" Aliniuliza.

"Ndiyo Dokta" Nilimjibu nikisimama na kumpa mkono.

"Nina habari mbaya" Alianza kusema, "Ni bora uketi" aliniambia

Niliketi. Daktari aliniambia kuwa Zuwena alikuwa kwenye koma na hakuna uwezekano wa kuwa mzima tena. Pia aliniambia kuwa wakati wakifanya vipimo vyao waligundua kuwa hali ya mtoto bado ni mzima.

(Inaendelea wiki ijayo)

DA:JESSY— KUJIANDAA KWA NDOA—1

Na. Jessica Fundi



Niandike leo kuhusu suala moja la kijamii ambalo naamini lina umuhimu wa pekee katika kujenga familia zenye nguvu, upendo, umoja na zitakazodumu.

Kati ya vitu ambacho mwanadamu anakutana navyo katika maisha yake hakuna kikubwa kama kuchagua ni nani mtu anataka kumchagua kuwa mwenzi wa maisha yake yote yaliyobakia.

Uamuzi huo ni mkubwa kuliko uamuzi wa shule, kazi, au mahali pa kuishi. Ni uamuzi unaohusu nani wa kuishi naye katika maisha.

Katika mfululizo huu nitaangalia kwa kidogo tu lakini kwa kina juu ya suala la kujiandaa kwa ndoa, yaani ni vitu gani vya msingi ambavyo mtu anatakiwa kujiandaa navyo kwa maisha ya unyumba.

Mara nyingi mtu anapofikiria suala la ndoa wanajiandaa kwa kuhakikisha wana ajira nzuri, nyumba nzuri na samani za kutosha na zaidi ya yote wanaziandaa familia zao kwwa wakwe wanaokuja na hivyo wanapoona kuwa mambo yako sawa basi hufanya harusi na kuanza maisha ya ndoa.

Hata hivyo baadhi ya watu (Marekani karibu nusu ya wana ndoa) huishia kupeana talaka ndani ya miaka michache ya mwanzo baada ya kugundua mambo ambayo hawakujiandaa nayo kabla.

Matokeo yake ndoa zinageuka kuwa kama magereza au vifungo vya maisha (labda ndiyo maana inaitwa kufunga pindu!) na mtu anajikuta analazimika kuishi kwenye ndoa yenye maumivu, na machungu mengi na hata wengine hufikia mahali pa kuanza kukimbia ndoa zao.

Ninaamini tatizo kubwa ni kuwa watu wengi waliofunga ndoa walijiandaa kwa vitu vingi sana isipokuwa kitu kimoja ambacho ndicho cha kwanza na cha msingi wa maandalizi mengine yote.

Ni kitu ambacho kama mtu hatajiandaa nacho, basi atakuwa hajajiandaa kwa kwa ndoa bali labda kwa harusi na sherehe tu.

Tutaendelea wiki ijayo na kitu hicho cha kwanza.

Niandikie: dajessy@klhnews.com

MAWAZO MBADALA

Cheche inatoa nafasi kwa kiongozi yeyote wa CCM au mgombea wake Busanda kujibu hotuba ya Zitto ambayo imechapishwa kwenye kijarida hiki.

Majibu hayo yawe ndani ya kurasa kama tatu na yatahariri wa kutosha kurasa mbili za kijarida chenu. Tuma: mhariri@klhnews.com


MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

KATUNI ZA WIKI

Picha ya Wiki



Lori kwenyee matope huko Muhoro Rufiji. Je Taifa leto limekwama kwenye tope la ufisadi, na sisi watazamaji?





PATA HABARI MOTOMOTO NA MIJADALA

http://www.mwanakijiji.com

Jiandikishe kushiriki mijadala, kupata habari, kusikiliza muziki masaa 24 na matangazo ya moja kwa moja kila mwishoni mwa juma.

Ukizungumzia habari, unatuzungumzia

KUTOKA KWENYE MTANDAO

Uchaguzi Biharamulo, Julai 5

Mwisho wa Utezi wa Wagombea ni Juni 9, kampeni Juni 10-Julai 4, Uchaguzi Julai 5.Uchaguzi huo unafuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo Hilo, Pheres Kabuye, kilichosababishwa na ajali ya gari mkoani Morogoro.

Huu ni uchaguzi mwingine wa moto kati ya TLP kuthibitisha sio chama mfu kwa kutetea kwa nguvu zote, kiti pekee cha ubunge kilichoshikwa na chama hicho, Chadema lazima ifanya tena kipimo cha operesheni Sangara huku CUF iking'ng'na na Ngangari yake wakati CCM watataka kumaliza usongo wa kulikosa jimbo hilo kwa kipindi kirefu.

Matokeo yatakuwa yale yale kama tutakayoyashuhudia Busanda hivi karibuni, watagawana kura nyingi hivyo kumpa mwanya mgombea wa CCM kushinda kwa kura chache na mwisho wa yote, "The winner takes it all'

Kwa wapinzani kutoungana na kumsimamisha mgombea mmoja, ni CCM Busanda, CCM Biharamulo na 2010 ni CCM kwa kwenda Mbele.—**Pasco**

Ufisadi kila sehemu kuanzia kwenye halmashauri mpaka kwenye Taifa. ndio maana wanapata kigugumizi kuwajibishana. mambo mengine ni bora kutoyajua kuliko kuyajua yanaumiza sana - **Qute**

Mkuu Mwanakijiji,
Nashukuru sana kwa juhudi ya kuamsha fikra za watanzania.Hii juhudi unayofanya imeanza kuzaa matunda nakala zako najitahidi sana kuzigawa vijijini kyela kwa kuwatumia walimu wa kata.—**Nsaji Mpoki**

Ripoti ya CAG ina-base katika vitabu vile alivyokabidhiwa tu. Jamaa wakiona kuna maroroso zaidi katika vitabu hata kuumbuka zaidi wanaficha. ndiyo maana unaona hicho kilichopo. zidi ni kuwa pamoja na kuficha hayo maroroso mengine hayajifichi.

Sasa fikiri ;
Maroroso yalitolewa + Maroroso yaliyofichwa = kitu gani? - **Akajase**

TOA NAKALA MOJA

Cheche za Fikra
Mchapishaji na Mhariri Mtendaji

M. M. Mwanakijiji

Timu ya Waandishi
Benjamin Mwalukasa— Mhariri

Freddy Katunzi—Habari za Siasa

Mahmoud Rashid—Habari mbalimbali

Jessica L. Fundi – Makala

Kwa kujiandikisha,
maoni, habari, na ushauri

Tuandikie:
mhariri@ klhnews.com

Tovuti: http://www.mwanakijiji.com

***Kanusho:** Mawazo yanayonukuliwa hayawakilishi msimamo au mawazo ya mchapishaji na utawala wa kijarida hiki.*